
HABARI NJEMA



Kwa Ulimwengu Wa Habari Mbaya






Aliumba mtu kwa sura yake.Hakukua na uchungu,Hakukua na kuumia wala mauti. Mungu akamwambia mtu kwamba anaweza kula chochote katika Shamba la Eden isipokuwa matunda kutoka kwa: mti wa ujuzi wa mema na mambaya.'' Mwanzo 2:17



Ibilisi ambaye ni malaika mwovu na alianguka, akaja kwa mwanamke akiwa ndani ya mwili wa nyoka mrembo na kumjaribu ili ale tunda lililokatazwa.





Mke wa Adamu, Hawa, akala tunda Na akampa mumewe. Mtu alipomwasi Mungu, jambo mbaya Sana lilitendeka kwao na kwetu.



Mungu alikuwa amewaonya kwamba wasipotii, wangekufa. Adam alikula na kuleta laana mbaya ya kifo juu ya wanadamu wote na hata ufalme wa wanyama.

Adamu na Hawa wakatenganishwa na ushirika na Mungu aliewaumba na kuwapenda. Watu sasa wanaishi katika mgogoro mmoja na mwingine na chini ya haibu na huzuni ya moyo wa mwanadamu wenye thambi.






Kwa sababu ya thambi, Adamu na Hawa walifukuzwa kutoka kwenye shamba nzuri ambalo Mungu alikuwa amewandalia. Lakini Mungu bado aliwapenda na akawavarisha ngozi ya mnyama asie na hatia.



Adamu na Hawa hawakuwa wameona mauti hapo mbeleni. Mungu alikuwa ana waonyesha ya kwamba kondoo asiye na hatia lazima angekufa kwa anjiri ya thambi ya wenye kuhukumika.




Katika agano la Kale, watu wangekuja kwa Mungu kwa imani kupitia thambihu za wanyama wasio na hatia ambazo zilielekezwa kwa thambihu kuu ambayo siku moja ingetolewa kuondoa thambi.

Huzuni kuu ya Adamu na Hawa ingekuja wakati mwana wao mkumbwa, Kaini angemua ndugu yake mdogo Habili, kwa sababu ya hasira na wivu. Thambi ni kitu kibaya na kimeacha kovu isiopendeza ya fujo ya mwanadamu.



HABARI MBAYA: “Mshahara wa thambi ni mauti.” Warumi 6:23




Mwanadamu mwenye thambi zaidi, na mara fujo ikajaa ulimwenguni. Kupitia kwa Nuhu Mungu aliwaonya watu kuwa hukumu ilikuwa ukuje uliomwenguni. Lakini watu wakamdhihaki Nuhu na kukataa ujumbe wa Mungu.



Hatimaye' ile meli kubwa ambayo Mungu alimwambia Nuhu aijenge ikakamilika. Na yeye na jamii yake pamoja na maelfu ya wanyama wakawa na makao ndani yake. Hukumu ilikuwa inakuja!



Biblia inatwambia Mungu alituma mafuriko ulimwenguni mzima. Ni Nuhu na jamii "Walipata neema machoni pa Bwana''kwa sababu waliamini yale Mungu alikuwa amewaambia.



Baada ya siku arobaini mchana na arobaini usiku, mvua ikaacha kunyesha. Safina hatimaye ikatulia juu ya ''mlima ya Ararat'' mwaka mmoja baada ya mafuriko kuanza.



Baada ya kutoka kwenye safina, jambo la kwanza Nuhu alifanya ni kujenga madhabahu kwa Bwana na kutoa thabihu ya mnyama asiye na hatia kama malipo ya thambi zake na jamii yake.

Miaka nyingi baadaye Mungu alimchagua mtu aliyeitwa Abrahamu kuzaa taifa ambalo lingetoa neno la Mungu na sheria za Mungu.

Wakati huu,wale waliomjua Mungu waliendelea kutoa thabihu ya wanyama wasio na hatia kwa BWANA kama thabihu kwa ajili ya thambi zao. Lakini damu ya wanyama haingeondoa hukumu ya thambi za mwanadamu, na siku ingekuja ambapo Mungu angetoa dhabihu kuu. Dhabihu hiyo kamili na haina thambi ingekuja ulimwenguni kufa kuajili ya thambi za wanadamu!




Siku moja, Abrahamu, baba wa wayahudi, aliambiwa na Mungu aende mlimani akaabudu nakutoa dhabihu ya thambi.



Abrahamu alijaribiwa sana na Mungu alipoambiwa amtoe mwana wake juu ya madhabahu Kama dhabihu ya thambi.




Lakini Mungu alitoa kondoo mume amenaswa kwenya kichaka kama mbadala wa isaka. Hii ilikuwa ni hakikicho kuwa Mungu angetoa mwana wake afe kama dhabihu mahali petu!



Mungu alikuwa akimwonyesha Abrahamu siku za usoni Kodoo wa Mungu aliekamilika angekufa na kuosha thambi zote za kila mtu ambae angeweka imani yake kwake.



Miaka mingi badaye, katika nchi ya Misiri, Mungu aliwaambia watu wake wapake damu ya kondoo wa Pasaka kwenye vizingiti vya mulango Ili waweze kutoroka hukumu ambayo ilikuwa ina kuja juu ya wasioamini. Kutoka 12:1-13



Wakati huo, Mungu alimpa Musa sheria kwa ajili ya waebrania ili watu wote wajue wema na ubaya na kuwaonyesha kuwa walihitaji mwokozi. Kila mtu ni mwenye dhambi kwa kuzaliwa na kwa kuchagua na hakuna mtu anaweza kuweka mambo matakatifu ya sheria za Mungu, Amri kumi.

Amiri kumi za Mungu:
1. Usiwe na Mungu mwingine kando Yangu. 2. Usichonge sanamu yoyote na kuabudu. 3. Usitanje jina la Mungu wako kwa mzaha. 4. Ikumbuke sabato na uiweke takatifu.
5. Mheshimu baba na mama yako. 6. Usiue. 7. Usizini. 8. Usiibe. 9. Usishuhudie uongo. 10. Usitamani Mali ya mwenzio.



Kwa miaka mingi dhabihu za kila mara za kodoo wasio na hatia zilionyesha matokeo ya thambi ambayo ni mauti.

Lakini dhabihu za wanyama hazingeweza kuodoa adhabu ya dhambi za mwandamu ... Ingechukua dhabihu kuu Ambaye angeitwa mwana kodoo.


Nabii wa agano la kale kwa jina Isaya alitabiri bikira atatunga mimba na kuzaa mwokozi ambaye angefanyika dhabihu kwa ajili ya thambi za watu. Isaya 7:14.




Hatimaye miaka mingi baadaye, malaika alikuja na akatangaza habari hizi njema kwa msichana bikira alieitwa Mariamu alieishi katika mji wa Nazareti katika nchi ya Israeli. Kuzaliwa kwa mwana wa Mungu kungekuwa muujiza. Hangekuwa na baba mwanadamu.




Mwokozi alizaliwa katika hori huko Bethrehemu. **Mungu alikuwa amefanyika mwanadamu!** Jina lake ilikuwa Yesu na angeitwa mwana Kodoo wa Mungu. Yesu angewaokoa wengi kutokana na adhabu na nguvu za dhambi zao.



Yesu alipokua na kuanza huduma yake, alionyesha upendo wake huruma Kwa watu wote. Aliwaponya wagonjwa na kuwapa kuona vipovu waliokuja kwake Kwa imani. Yesu alikuwa na nguvu zote juu ya mapepo wachafu na bado ana nguvu hizo hizo leo.



Yesu alitenda miujiza mingi. Wakati mmoja alishangaza umati alipowalisha wote na chakula cha mvulana mdogo cha samaki wawili na mikate mitano midogo.



Yesu hata alifufua wafu aliposema- ''Lazaro toka.''


Yesu alitangaza – "Mimi ndiye ufufuo, na uzima' yeyote anayeniamini hata kama amekufa, ataishi tena'' Yohana 11:25




Yesu alikuwa na nguvu juu ya upepo na mawimbi, kuonyesha kuwa alikuwa mwana wa Mungu, muumba wa mbingu na dunia. Mariko 4:35-41 Yohana 1:1-3



Kama vile Yesu alivyotuliza bahari yenye hamaki, anaweza kuleta amani kwa moyo uliosumbuka uliowekwa kovu na shida na majaribu ya maisha.




Hata baada ya wema wote alioutenda, Yesu alichukiwa na viongozi wadini. Walimkamata kumshutumu vibaya. Watu waovu walimtemea mate, wakampiga na kuweka kofia ya mimba juu ya kichwa chake, na kumpeleka akasulubiwe.



Yesu alisulubiwa juu ya masalaba kama mharifu yeyote, Mwana wa Mungu aliteseka na kufa kulipa ghalama ya dhambi zetu zote.




Kama vile Mungu alivyoahidi, Kodoo wa Mungu mtakamilifu, asie na hatia alikufa kama dhambihu mahali petu!



Mmoja wa wahalifu aliekufa karibu na Yesu akamwomba mwokozi amkumbuke atakapo kuja kwa ufalme wake. Yesu akmwambia "leo utakuwa nami paradiso." Luke 23:43 Mwizi aliekuwa anakufa alijua angeishi milele na Yesu alipokufa. Nijambo la ajabu kujua kuwa unaweza kuwa wa milele Kwa kuliitia jina la Yesu Kristo!

"Kila atakaye liitia jina la Bwana ataokoka." Warumi 10:13



Kabla hajafa, Yesu aliomba— “Baba wasamehe’’Hata askari wakirumi alijua kuwa huyu mtu aliyeombea maadui zake alikuwa mwana wa Mungu!



Baada ya kufa kwa ajili ya dhambi zetu, Yesu alizikwa katika kaburi jipya kwenye shamba lilo kuwa nje ya kuta za Jerusalem.



Askari wa kirumu wariamrishwa kulinda kaburi ili kusewe na mtu ambaye angeiba mwili wa Bwana Yesu Kristo.


Yesu alikaa kaburini siku tatu wakati wa Pasaka na sabato.

Ilikuwa ni wakati wa giza ya aina gani kwa wafuasi wa Yesu ambao walikuwa wamejificha kwa uoga. Katika huzuni na uoga wao walisahau kuwa Yesu alikua amewambia kuhusu kifo chake, kuzikwa na kufufuka, “Kama Yona alivyokuwa dani ya tumbo la samaki kwa siku tatu, vivyo hivyo mwana wa adamu angekaa siku tatu katika tumbo la ardhi.’’ Mathayo 12:40



Katika siku ya kwanza ya juma, Yesu alifufuka kutoka kwa wafu! Mwana wa Mungu alishinda dhambi na mauti!

Yesu alisema “Kwa sababu mimi ni hai, mtakuwa hai pia.’’ Yohana 14:19



Asubuhi ya siku ya ufufuo, kikundi cha wanawake waaminio walikuja kuupaka mafuta' mwili wa Yesu. Waliambiwa na malaika, "yeye hayuko hapa, amefufuka kutoka kwa wafu.'' Mathayo 28:1-6


Wanafunzi wa Yesu wawili walikimbia kwenda kwenye kaburi na wakashangaa kuwa nguo za kaburi bado zilikuweko, lakini Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu! Yohana 20:1-8




Katika ulimwengu wetu unaja mauti na giza. Kufufuka kwa Yesu Kristo kuna wapatia tumaini wote wanao mwamini yeye. Yesu yu hai na anaahidi kipawa cha uzima wa milele wote waonao mtumaini kama mwokozi.

Ni Yesu tu anaweza kupeana uzima wa milele, kama alivyosema "Mimi ndiye njia, ukweli na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia yangu mimi.'' Yohana 14:6

Unaweza kupokea kipawa cha uzima wa milele kama utagairi dhambi zako na kutoamini na kumtumaini kama mwokozi wako!



Baada ya kufuka kwake, alijitokeza kwa wafuasi wake na waumini wengine. Hata aliomba kitu ale ilikuwaonyesha kuwa mwili wake ulikuwa umefufuliwa na kwamba kweli alikuwa hai! Luka 24:36-43



Baada ya siku arobaini, Yesu alirudi mbinguni, lakini kabla hajaoodoka, Aliahindi kuwa siku moja angerundi duniani kwa ajili ya wafuasi wake! Yesu alisema—"naenda kuwaadalia mahali. Nitakuja tena, niwakaribishe kwangu, Ili nilipo Mimi, nanyi mwepo." Yohana 14:2-3



Mwana aliyefufuka na kutukuzwa wa Mungu sasa ameketi mkono wa kuume wa Baba yake mbinguni.Yeye diye mwombezi na wakili wa wote wanaomtumaini kama mwokozi wetu!

HABARI MBAYA: "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti "

HABARI NJEMA: " . . . Lakini karama ya Mungu ni uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo. Bwana wetu." Warumi 6:23

Tunapotambua dhambi zetu na kweli kuamini kuwa Bwana Yesu alikufa kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu, sote tunapewa karama ya bure ya uzima wa milele na majina yetu yanaadikwa katika Kitabu cha uzima cha "Mwana Kondoo" Ufunuo 20:11-15

"Yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa."Warumi 10:13

Yesu alizibeba dhambi za ulimwengu juu yake alipotoa uhai wake msalabani. Tunapomtumaini kama mwokozi wetu, anatusamehe na kutufunika kwa haki yake—

“Yeye asiyejua dhambi, alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ilisisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye.”
2 Wakorintho 5:21



“Nitafurahi sana katika Bwana, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana amenifunika mavazi ya wokovu… Amenifunika mimi na vazi ya utukufu wake.”
Isaya 61:10

Swali: Kuna chochote kinachokuzuilia kuomba na kumpokea Yesu Kristo kama mwokozi sasa hivi?

“Itamfaidi nini mtu kupata ulimwengu wote, na apoteze nafsi yake?” Mariko 8:36

Kama umeamini Bwana Yesu Kristo alikufa kwa anjili yako na ungependa akuokoe kutokana na dhambi zako, tunapendekeza ombi hili au lingine linalofanana na hili kwa maneno yako mwenyewe:

“Bwana Yesu, najua ya kwamba nimetenda thambi na sitahili kuishi nawe milele mbinguni. Lakini naamini ulikufa msalabani kulipia thambi zangu.

Kwa imani nageuka kutoka kwa kutoamini kwangu na kuomba uniokoe. Nakukaribisha katika maisha yangu.

Asante kwa kunipenda, na kunifia msalabani. Asante kwa kunipatia karama ya mungu ambayo ni uzima wa milele. Nisaindie sasa kusoma neon lako na kukuishia.

Katika jina la Yesu’ nimeomba, Amina.”

“Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminilo jina Lake. Yohana 1:12

“Kwasabu ukimkiri Yesu kwa kinyua chako, ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako yakuwa Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinyua kukiri hata kupata wokovu.” Warumi 10:9-10

Tunakutia moyo usome neno la Mungu, Bibilia kila siku…na utafute kanisa ambayo inafundisha Bibilia aya kwa aya kwa uaminifu. Kubatizwa kwa maji hakutamwokoa yeyote, lakini ni amri ya Mungu na ushuuda kwa wengine kwamba umemwamni kristo. Shiliki na waumini wengine katika Yesu na uwaambie wengine kile Yesu amekutendea…na amewatendea.

Bibilia inatangaza kuwa unaweza kujua una uzima wa milele kwa kumwamini Yesu Kristo'.

"Mwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaokolewa pamoja na nyumba yako." Mitume 16:31

"Nimewandikia ninyi mnaloamini jina la mwana wa mungu ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele..." 1 Yohana 5:13

"Amwaminiye mwana ana uzima wa milele; asiyeamini mwana hataona uzima bali adhambu ya mungu inamkalia." Yohana 3:36

"Amini, amini, nawambia, yeye alisikiaye neno langu na kumwamini ye aliyenituma, ana uzima, wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mauti na kuingia uzimani." Yohana 5:24

"Sasa basi, hakuna adhukumu juu yao walio katika Kristo Yesu." Warumi 8:1

"Kwa maana mmekuja kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliopo, wala yatakayokuwepo, wala uwezo, wala yaliojuu, wala yaliochini, wala kiumbe kinginecho chochote hakitaweza kututenganisha na upendo wa mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana." Warumi 8:38-39